**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA ELIMU SAYANSI NA TEKNOLOJIA**

# MUHTASARI WA SOMO LA KISWAHILI
# ELIMUMSINGI DARASA LA III-VI
# SHULE ZINAZOTUMIA LUGHA YA KIINGEREZA KUFUNDISHIA

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU SAYANSI NA TEKNOLOJIA

# MUHTASARI WA SOMO LA KISWAHILI
# ELIMUMSINGI DARASA LA III-VI
# SHULE ZINAZOTUMIA LUGHA YA KIINGEREZA KUFUNDISHIA

©Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, 2016

Toleo la kwanza, 2016

ISBN. 978-9976-61-598-2

Taasisi ya ElimuTanzania
S. L. P. 35094
Dar es Salaam.
Simu:+255 22 2773005/+255 22 277 1358
Faksi: +255 22 2774420
Baruapepe:director.general@tie.go.tz
Tovuti: www.tie.go.tz

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kuiga, kunakili, kutafsiri, kupiga chapa au kutoa andiko hili kwa namna yoyote ile bila idhini ya Kamishna wa Elimu,Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

## YALIYOMO


Ukarasa

Dibaji ........................................ v
1.0 Utangulizi........................................ 1
2.0 Maelezo ya Jumla Kuhusu Mtaala ........................................ 1
2.1 Malengo ya Elimumsingi Darasa la III - VI ........................................ 1
2.2 Umahiri wa Elimumsingi Darasa la III-VI ........................................ 2
2.3 Malengo ya Somo la Kiswahili katika Elimumsingi Darasa la III - VI ........................................ 3
2.4 Umahiri wa Somo la Kiswahili ........................................ 3
2.5 Ufundishaji na Ujifunzaji wa Somo la Kiswahili ........................................ 4
2.6 Upimaji wa Ujifunzaji ........................................ 4
3.0 Maudhui ya Muhtasari ........................................ 4
3.1 Umahiri Mkuu ........................................ 4
3.2 Umahiri Mahususi ........................................ 5
3.3 Shughuli za Kutendwa na Mwanafunzi ........................................ 5
3.4 Vigezo vya Upimaji ........................................ 5
3.5 Viwango vya Utendaji ........................................ 5
3.6 Idadi ya Vipindi ........................................ 5
3.7 Maudhui ya Darasa la III ........................................ 6
3.8 Maudhui ya Darasa la IV ........................................22
3.9 Maudhui ya Darasa la V ........................................ 36
3.10 Maudhui ya Darasa la VI ........................................50

## Dibaji

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ilifanya mabadiliko ya Sera ya Elimu mwaka 2014. Mabadiliko hayo yamefanya kuwe na mabadiliko katika mtaala wa elimumsingi ili kuleta ufanisi katika utekelezaji wake. Baadhi ya masomo yameboreshwa na mengine mapya kuingizwa katika mtaala wa darasa la III – VI. Kutokana na mabadiliko hayo Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imeandaa Muhtasari huu wa somo la Kiswahili ili kukidhi mahitaji ya Sera ya Elimu na Mafunzo.

Muhtasari huu unasisitiza kufundisha na kujifunza kunakozingatia ujenzi wa umahiri kwa mwanafunzi. Mwalimu halazimiki kufuata mtiririko wa umahiri uliopo katika muhtasari huu ila ana wajibu wa kuhakikisha kwamba uhusiano kati ya umahiri mmoja hadi mwingine unazingatiwa. Katika kuandaa azimio la kazi mwalimu azingatie uwezo na mahitaji ya mwanafunzi katika kujifunza.

Msisitizo umewekwa ili kumsaidia mwanafunzi kujenga stadi za kusikiliza, kuzungumza, kusoma na kuandika. Mwalimu anasisitizwa kutumia vigezo vya upimaji na viwango vya kupima utendaji wa mwanafunzi vilivyoanishwa katika Muhtasari huu. Kwa hiyo upimaji wa Somo la Kiswahili utajikita zaidi katika viwango vya utendaji wa mwanafunzi katika kukuza maarifa, stadi na mwelekeo kama inavyotarajiwa.

Ni matarajio yangu kuwa Muhtasari huu utamwezesha mwalimu kufanya kazi yake kwa ufanisi. Kwa kuwa uboreshaji wa mihtasari ni mchakato endelevu, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia inaendelea kupokea maoni ya kuboresha muhtasari huu kutoka kwa walimu na wadau wengine wa elimu. Maoni yote yapelekwe kwa Mkurugenzi Mkuu, Taasisi ya Elimu Tanzania.



Prof. Eustella P. Bhalalusesa
**Kamishna wa Elimu**
**Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia**

## 1.0 Utangulizi

Muhtasari huu wa Somo la Kiswahili umeandaliwa kutokana na Mtaala wa Elimumsingi wa Darasa la III - VI wa mwaka 2016. Muhtasari huu umegawanyika katika sehemu kuu tatu. Sehemu ya kwanza ni utangulizi, sehemu ya pili inahusu Malengo ya jumla ya mtaala na sehemu ya tatu ni maudhui ya muhtasari.

Somo la Kiswahili linafundishwa katika ngazi ya Elimumsingi kuanzia Darasa la III hadi la VI. Somo hili ni muhimu kufundishwa ili kukuza uwezo wa kuwasiliana katika mazungumzo na maandishi. Katika shule zinazotumia lugha ya Kiingereza kufundishia, somo hili limekuwa likifundishwa bila kuweka msisitizo katika kuwajengea wanafunzi stadi za msingi za kusoma, kuandika na kuhesabu. Hivyo, katika muhtasari huu, stadi hizi zimewekewa msisitizo kwani ni msingi muhimu katika kumwezesha mwanafunzi kumudu maudhui ya somo la Kiswahili kwa ngazi ya Darasa la III hadi ngazi za juu. Nchini Tanzania Kiswahili kimepewa hadhi ya kuwa lugha rasmi na lugha ya Taifa. Kwa ujumla, Kiswahili ni kichocheo cha uzalendo na umoja wa kitaifa kwa Watanzania.

## 2.0 Maelezo ya Jumla Kuhusu Mtaala

Mtaala wa Elimu msingi Darasa la III -VI umeundwa na sehemu mbalimbali ambazo zinaonesha kwamba mtaala ni dhana inayojumuisha mambo mengi ambayo yanahusiana. Sehemu hii inawasilisha baadhi ya vipengele vya mtaala ambavyo ni Malengo ya Elimumsingi, umahiri wa Elimumsingi Darasa la III-VI, malengo ya somo la Kiswahili, umahiri mkuu na mahususi, ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili na upimaji wa ujifunzaji.

### 2.1 Malengo ya Elimumsingi Darasa la III-VI

Elimumsingi Darasa la III–VI ina madhumuni ya kuwapatia walengwa maarifa, stadi na mielekeo inayohitajika kwa maendeleo ya Watanzania. Yafuatayo ndiyo malengo makuu ya Elimumsingi Darasa la III – VI:

a) Kumwezesha mwanafunzi kukuza stadi za kusoma, kuandika, kuhesabu na kuwasiliana.

b) Kumwezesha mwanafunzi kuifahamu, kuitumia na kuithamini lugha ya Kiswahili.

c) Kumwezesha mwanafunzi kufahamu misingi ya utawala wa sheria.

d) Kumwezesha mwanafunzi kuthamini utamaduni wa Kitanzania na wa jamii nyingine.
e) Kukuza uwezo wa mwanafunzi kufikiri, kubuni na kutatua matatizo.
f) Kumwezesha mwanafunzi kutambua umuhimu wa maadili, uadilifu na uwajibikaji kama misingi ya raia mwema.
g) Kumwezesha mwanafunzi kushiriki katika shughuli za michezo na sanaa pamoja na kuthamini kazi za kisanii.
h) Kumwezesha mwanafunzi kubaini na kukuza vipaji na vipawa vyake.
i) Kumwezesha kila mwanafunzi kuthamini na kupenda kufanya kazi.
j) Kumwezesha mwanafunzi kutambua, kuthamini na kutumia teknolojia na ufundi.
k) Kumwandaa mwanafunzi kwa ngazi nyingine ya elimu pamoja na kujifunza kusiko na kikomo.

## 2.2 Umahiri wa Elimumsingi Darasa la III-VI

Umahiri wa Elimumsingi umejikita katika kumwandaa mwanafunzi wa Darasa la III hadi laVI kuwa na uwezo wa:

a) Kuwasiliana kwa ufasaha kwa lugha ya Kiswahili na Kiingereza kwa kuzungumza na kuandika.
b) Kusoma kwa kujiamini na kwa ufahamu.
c) Kutumia dhana na kanuni za kihisabati katika maisha ya kila siku.
d) Kutumia stadi za kisayansi, kiteknolojia na ufundi katika maisha ya kila siku.
e) Kuthamini utamaduni wake na wa jamii nyingine.
f) Kujali tofauti za kiimani na kiitikadi katika jamii.
g) Kushiriki katika michezo na shughuli za kisanii.
h) Kujiheshimu na kuwaheshimu wengine.
i) Kutenda matendo ya kizalendo.
j) Kushiriki katika kazi mbalimbali zinazoendana na umri wake.
k) Kushiriki katika shughuli zinazokuza uwezo wake wa kufikiri kimantiki na kiyakinifu.
l) Kushirikiana na wengine kwa kufanya matendo yanayokubalika katika jamii.

## 2.3 Malengo ya Somo la Kiswahili katika Elimumsingi Darasa la III-VI

Ufundishaji wa somo la Kiswahili katika Elimumsingi Darasa la III - VI umelenga kumwezesha mwanafunzi:-

a) Kuzungumza, kusikiliza, kusoma na kuandika kwa kutumia lugha ya Kiswahili.
b) Kutumia Kiswahili fasaha katika miktadha mbalimbali.
c) Kutumia Kiswahili kupata maarifa, stadi na mwelekeo wa kijamii, kiutamaduni, kiteknolojia na kitaaluma kutoka ndani na nje ya nchi.
d) Kukuza stadi za mawasiliano ili kumwezesha mwanafunzi kumudu maisha yake.
e) Kujenga msingi bora na imara wa kujifunza kwa ajili ya elimu ya juu na kujiendeleza binafsi kwa kutumia lugha ya Kiswahili.
f) Kuifahamu, kuitumia na kuithamini lugha yaTaifa.

## 2.4 Umahiri wa Somo la Kiswahili

Sehemu hii inabainisha umahiri utakaojengwa na mwanafunzi wa Darasala III- VI katika somo

| | Umahiri Mkuu | Umahiri Mahususi |
|---|---|---|
| 1. | Kuwasiliana katika miktadha mbalimbali. | 1.1 Kutambua sauti mbalimbali katika matamshi ya silabi, maneno, sentensi na habari.<br>1.2 Kuanzisha na kuendeleza mazungumzo katika miktadha mbalimbali.<br>1.3 Kutumia maandishi katika mawasiliano kulingana na miktadha mbalimbali. |
| 2. | Kuonesha uelewa wa jambo alilolisikiliza au kulisoma. | 2.1 Kusikiliza na kuonesha uelewa wa jambo alilolisikiliza.<br>2.2 Kusoma kwa ufasaha na kuonesha uelewa wa matini aliyoisoma. |
| 3. | Kutumia msamiati katika miktadha mbalimbali | 3.1 Kuzungumza kwa kuwasilisha hoja kulingana na miktadha mbalimbali.<br>3.2 Kutumia maandishi katika kuandaa matini mbalimbali.<br>3.3 Kusoma na kuchanganua mawazo yaliyowasilishwa katika matini mbalimbali. |

## 2.5 Ufundishaji na Ujifunzaji Somo la Kiswahili

Ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili utaongozwa na ujenzi wa umahiri kwa kutumia mbinu shirikishi. Mbinu hizi zitamfanya mwanafunzi kuwa kitovu cha kujifunza na mwalimu kuwa mwezeshaji. Aidha, ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili kwa shule zinazotumia lugha ya Kiingereza kufundishia utakuwa na shughuli nyingi za kutenda ambazo zitajumuisha stadi za kusoma na kuandika. Stadi hizi ni muhimu kwao kwa sababu ni mara yao ya kwanza kujifunza kwa kutumia lugha ya Kiswahili. Hivyo wanafunzi wataweza kupata maarifa, stadi na mwelekeo ulio sawa na wanafunzi wanaotumia lugha ya Kiswahili kujifunzia na kuweza kufanya vizuri mtihani wa Somo la Kiswahili Darasa la IV. Vile vile mwanafunzi ataweza kutumia lugha ya Kiswahili kwa ufasaha katika kusikiliza, kuzungumza, kusoma na kuandika anapomaliza Elimumsingi Darasa la III-VI.

## 2.6 Upimaji wa Ujifunzaji

Upimaji ni kipengele muhimu katika mchakato mzima wa ufundishaji na ujifunzaji. Upimaji wa somo la Kiswahili utafanyika sambamba na masomo mengine yanayofundishwa katika elimumsingi. Upimaji huu utamwezesha mwalimu kupima umahiri wa mwanafunzi wa kujieleza kwa ufasaha katika miktadha mbalimbali, kusikiliza, kusoma kwa ufasaha, kutafsiri, kujibu maswali ya habari aliyoisoma, kuandika sentensi, habari fupi na hadithi kwa kuzingatia kanuni za uandishi. Aidha utamwezesha mwalimu kubaini uwezo wa wanafunzi wa kutumia msamiati sahihi katika miktadha mbalimbali. Zana zifuatazo zitatumika katika upimaji wa somo la Kiswahili; mkoba wa kazi, majaribio, hojaji, orodha hakiki, kazi mradi, mitihani ya muhula pamoja na fomu ya ufuatiliaji.

## 3.0 Maudhui ya Muhtasari

Maudhui ya Muhtasari yamepangwa kwa kila darasa yakihusisha umahiri mkuu, umahiri mahususi, shughuli za kutendwa na mwanafunzi, vigezo vya upimaji, viwango vya utendaji na idadi ya vipindi.

## 3.1 Umahiri Mkuu

Umahiri mkuu ni uwezo wa kutenda jambo kwa usahihi na kwa ufanisi unaokusudiwa kufikiwa na mwanafunzi baada ya kujifunza kwa muda fulani. Umahiri mkuu hujengwa na umahiri mahususi kadhaa atakaoujenga mwanafunzi kwa kutenda shughuli mbalimbali.

### 3.2 Umahiri Mahususi
Ni uwezo unaojengwa na mwanafunzi katika kutenda shughuli mbalimbali kwa muda maalumu.

### 3.3 Shughuli za Kutendwa na Mwanafunzi
Ni vitendo ambavyo mwanafunzi anapaswa kuvifanya ili kufikia umahiri mahususi uliokusudiwa kwa kuzingatia uwezo na umri wake.

### 3.4 Vigezo vya Upimaji
Ni viwango vya ufanisi wa utendaji wa mwanafunzi ili kufikia umahiri mahususi.

### 3.5 Viwango vya Utendaji
Ni kiasi cha ufikiwaji wa vigezo kwa kila shughuli anayotenda mwanafunzi.

### 3.6 Idadi ya Vipindi
Ni makadirio ya muda utakaotumika katika kufundisha na kujifunza kwa kuzingatia uzito wa umahiri mahususi na shughuli za kutendwa na mwanafunzi. Makadirio hayo ya muda yamewekwa kwa mfumo wa vipindi ambapo kila kipindi ni dakika 40. Somo hili litafundishwa kwa vipindi saba (7) kwa Darasa la III – IV na vipindi vitano (5) kwa Darasa la V-VI kwa wiki katika shule zinazotumia lugha ya Kiingereza kufundishia. Hata hivyo mapendekezo haya ya idadi ya vipindi yanaweza kubadilika kulingana na mazingira ya kufundishia na kujifunzia.

### 3.7 Maudhui ya Darasa la III

Umahiri Utakaojengwa na Mwanafunzi katika Somo

| | Umahiri Mkuu | Umahiri Mahususi |
|---|---|---|
| 1. | Kuwasiliana katika miktadha mbalimbali | 1.1 Kutambua sauti mbalimbali katika matamshi ya silabi, maneno, sentensi na habari<br>1.2 Kuanzisha na kuendeleza mazungumzo katika miktadha mbalimbali<br>1.3 Kutumia maandishi katika kuwasiliana kulingana na miktadha mbalimbali |
| 2. | Kuonesha uelewa wa jambo alilolisikiliza au kulisoma | 2.1 Kusikiliza na kuonesha uelewa wa jambo alilolisikiliza<br>2.2 Kusoma kwa ufasaha na kuonesha uelewa wa matini aliyoisoma |
| 3. | Kutumia msamiati katika miktadha mbalimbali | 3.1 Kuzungumza kwa kuwasilisha hoja kulingana na miktadha mbalimbali<br>3.2 Kutumia maandishi katika kuandaa matini mbalimbali<br>3.3 Kusoma na kuchanganua mawazo yaliyowasilishwa katika matini mbalimbali |

**Angalizo:** Katika jedwali la maudhui ya muhtasari kwenye kurasa zinazofuata umahiri mkuu wa kutumia msamiati katika miktadha mbalimbali hautasimama peke yake kama umahiri mkuu. Hivyo umahiri huo utajitokeza kama umahiri mahususi unaoingiliana na kila umahiri mahususi ndani ya umahiri mkuu wa kuwasiliana katika miktadha mbalimbali na umahiri mkuu wa kusoma kwa ufahamu katika kujenga uwezo wa kujieleza kwa namna mbalimbali.

**Jedwali la Maudhui ya Muhtasari**

| *Umahiri Mkuu* | *Umahiri Mahususi* | *Shughuli za Kutendwa na Mwanafunzi* | *Vigezo vya Upimaji* | *Upimaji wa Viwango vya Utendaji* | | | | *Idadi ya Vipindi* |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | *Utendaji wa awali wa Mwanafunzi* | *Utendaji wa wastani wa Mwanafunzi* | *Utendaji mzuri wa Mwanafunzi* | *Utendaji mzuri sana wa Mwanafunzi* | |
| 1. Kuwasiliana katika miktadha mbalimbali | 1.1 Kutambua sauti mbalimbali katika matamshi ya silabi, maneno, sentensi na habari fupi | a) Kuunda na kutamka silabi zinazotokana na herufi za irabu na konsonanti | Uundaji na utamkaji wa silabi zinazotokana na herufi za irabu na konsonanti unafanyika kwa usahihi | Anaunda silabi chache sana zinazotokana na herufi za irabu na konsonanti na kushindwa kuzitamka kwa usahihi | Anaunda silabi chache zinazotokana na herufi za irabu na konsonanti na kuzitamka | Anaunda silabi nyingi zinazotokana na herufi za irabu na konsonanti na kuzitamka | Anaunda silabi zote zinazotokana na herufi za irabu na konsonanti na kuzitamka | 30 |
| | | b) Kutamka sauti za maneno yanayoundwa na silabi sahili katika sentensi | Sauti za maneno yanayoundwa na silabi sahili katika sentensi yanatamkwa kwa usahihi | Anatamka sauti za maneno yanayoundwa na silabi chache sana | Anatamka sauti za maneno yanayoundwa na silabi sahili chache | Anatamka sauti za maneno yanayoundwa na silabi sahili nyingi | Anatamka sauti za maneno yanayoundwa na silabi sahili zote na kuunda silabi nyingine | |
| | | c) Kutamka sauti za herufi mwambatano (ny, nd, sh, ng, th, kw, mbw) na herufi nyingine zenye muundo, huo katika silabi, maneno, sentensi na habari fupi | Sauti za herufi mwambatano na herufi nyingine zinatamkwa katika silabi, maneno, sentensi na habari fupi kwa ufasaha | Anatamka sauti za herufi mwambatano chache sana katika silabi, maneno, sentensi na habari fupi | Anatamka sauti za herufi mwambatano chache katika silabi, maneno, sentensi na habari fupi | Anatamka sauti za herufi mwambatano nyingi katika silabi, maneno, sentensi na habari fupi | Anatamka sauti za herufi mwambatano nyingi sana katika silabi, maneno, sentensi na habari fupi na kuunda maneno mapya | |

| *Umahiri Mkuu* | *Umahiri Mahususi* | *Shughuli za Kutendwa na Mwanafunzi* | *Vigezo vya Upimaji* | *Upimaji wa Viwango vya Utendaji* | | | | *Idadi ya Vipindi* |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | *Utendaji wa awali wa Mwanafunzi* | *Utendaji wa wastani wa Mwanafunzi* | *Utendaji mzuri wa Mwanafunzi* | *Utendaji mzuri sana wa Mwanafunzi* | |
| | | d) Kutamka sauti za herufi mwambatano (dh, th, ng, mbw, ng', chw, ndw,) na herufi nyingine zenye muundo, huo katika silabi, maneno, sentensi na habari fupi | Sauti za herufi mwambatano na herufi nyingine zinatamkwa katika silabi, maneno, sentensi na habari fupi kwa ufasaha | Anatamka sauti za herufi mwambatano chache sana katika silabi | Anatamka sauti za herufi mwambatano chache katika silabi na maneno | Anatamka sauti za herufi mwambatano nyingi katika silabi, maneno, sentensi na habari fupi | Anatamka sauti za herufi mwambatano nyingi sana katika silabi, maneno, sentensi na habari fupi na kuunda maneno mapya | |
| | | e) Kutamka sauti za herufi mwambatano (gh,py,nz,ky,lw. pw,sw,tw) na herufi nyingine zenye muundo huo katika sentensi | Sauti za herufi mwambatano na herufi nyingine zimetamkwa katika silabi, maneno, sentensi na habari fupi kwa ufasaha | Anatamka sauti za herufi mwambatano chache sana katika sentensi kwa silabi na maneno | Anatamka sauti za herufi mwambatano chache katika silabi na maneno | Anatamka sauti za herufi mwambatano nyingi katika silabi, maneno, sentensi na habari fupi | Anatamka sauti za herufi mwambatano nyingi sana katika silabi, maneno, sentensi na habari fupi na kuunda maneno mapya | |
| | | f) Kuunda na kusoma sentensi zinazotokana na silabi za herufi mwambatano gh, py, nz, ky na silabi sahili | Sauti za herufi mwambatano gh, py, nz, ky na silabi sahili zimetamkwa katika silabi, maneno, sentensi na habari fupi kwa ufasaha | Anatamka sauti za herufi mwambatano chache sana katika silabi | Anatamka sauti za herufi mwambatano chache katika silabi n maneno | Anatamka sauti za herufi mwambatano nyingi katika silabi, maneno, sentensi na habari fupi | Anatamka sauti za herufi mwambatano nyingi sana katika silabi, maneno, sentensi na habari fupi na kuunda maneno mapya | |

| Umahiri Mkuu | Umahiri Mahususi | Shughuli za Kutendwa na Mwanafunzi | Vigezo vya Upimaji | Upimaji wa Viwango vya Utendaji | | | | Idadi ya Vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | *Utendaji wa awali wa Mwanafunzi* | *Utendaji wa wastani wa Mwanafunzi* | *Utendaji mzuri wa Mwanafunzi* | *Utendaji mzuri sana wa Mwanafunzi* | |
| | 1.2 Kutumia matamshi sahihi katika kutamka maneno mbalimbali | a) Kutamka maneno yenye herufi 's' na 'th' kwa usahihi | Maneno yenye herufi 's' na 'th' yametamkwa kwa usahihi | Anatamka maneno machache sana yenye herufi 's' na 'th' | Anatamka maneno machache yenye herufi 's' na 'th' | Anatamka maneno mengi yenye herufi 's' na 'th' | Anatamka maneno mengi sana yenye herufi 's' na 'th' na kuyatungia sentensi | 15 |
| | | b) Kutamka maneno yenye herufi 'z' na 'dh' | Maneno yenye herufi 'z' na dh' yanatamkwa kwa usahihi | Anatamka maneno machache sana yenye herufi 'z'. | Anatamka maneno machache yenye herufi 'z' na 'dh'. | Anatamka maneno mengi yenye herufi 'z' na 'dh'. | Anatamka maneno mengi sana yenye herufi 'z' na 'dh' mengi sana na kuyatungia sentensi | |
| | | c) Kutamka matamshi sahihi ya maneno yenye herufi'I' na 'r' | Maneno yenye herufi'l' na 'r' yanatamkwa kama ilivyokusudiwa | Anatamka maneno machache sana yenye herufi 'l' | Anatamka maneno machache yenye herufi 'l' na 'r' | Anatamka maneno mengi yenye herufi 'l' na 'r' | Anatamka maneno mengi sana yenye herufi ''l' na 'r' na kuyatungia sentensi | |
| | 1.3 Kuanzisha na kuendeleza mazungumzo katika miktadha mbalimbali | a) Kueleza shughuli anazofanya kwa siku | Shughuli zinazofanyika kabla ya kwenda shuleni, anapokuwa shuleni na anaporudi nyumbani zinaelezwa kwa usahihi | Anaeleza shughuli chache sana anazofanya kabla ya kwenda shuleni | Anaeleza shughuli chache anazofanya kabla ya kwenda shuleni na anapokuwa shuleni. | Anaeleza shughuli nyingi anazofanya kabla ya kwenda shuleni na anapokuwa shuleni na anaporudi nyumbani | Anaeleza shughuli zote anazofanya kabla ya kwenda shuleni, anapokuwa shuleni na anaporudi nyumbani kwa kutoa mifano. | 45 |

| *Umahiri Mkuu* | *Umahiri Mahususi* | *Shughuli za Kutendwa na Mwanafunzi* | *Vigezo vya Upimaji* | *Upimaji wa Viwango vya Utendaji* | | | | *Idadi ya Vipindi* |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | *Utendaji wa awali wa Mwanafunzi* | *Utendaji wa wastani wa Mwanafunzi* | *Utendaji mzuri wa Mwanafunzi* | *Utendaji mzuri sana wa Mwanafunzi* | |
| | | b) Kutumia lugha ya heshima kuomba ruhusa na kuomba vitu | Lugha ya heshima katika kuomba ruhusa na kuomba vitu inatumika kwa usahihi | Anatumia lugha ya heshimia kuomba ruhusa kwa baadhi ya mambo. | Anatumia lugha ya heshima kuomba ruhusa kwa baadhi ya mambo na kuomba baadhi ya vitu | Anatumia lugha ya heshima kuomba ruhusa na kuomba vitu | Anatumia lugha ya heshima kuomba ruhusa katika miktadha mbalimbali na kuomba vitu | |
| | | c) Kusimulia hadithi na kueleza mafunzo yanayopatikana | Hadithi zinasimuliwa na mafunzo yaliyomo yanaelezwa kwa usahihi. | Anasimulia hadithi na kueleza mafunzo machache sana ya hadithi hiyo | Anasimulia hadithi na kueleza mafunzo machache ya hadithi hiyo | Anasimulia hadithi na kueleza mafunzo mengi ya hadithi hiyo | Anasimulia hadithi na kueleza mafunzo yote ya hadithi hiyo kwa usahihi | |
| | | d) Kuelezea matukio yaliyooneshwa katika picha mbalimbali | Matukio mbalimbali yaliyooneshwa katika picha yameelezewa kwa usahihi | Anaelezea machache sana matukio yaliyooneshwa katika picha | Anaelezea matukio machache yaliyooneshwa katika picha | Anaelezea matukio mbalimbali yaliyooneshwa katika picha | Anaelezea matukio yote yaliyooneshwa katika picha | |

| Umahiri Mkuu | Umahiri Mahususi | Shughuli za Kutendwa na Mwanafunzi | Vigezo vya Upimaji | Upimaji wa Viwango vya Utendaji | | | | Idadi ya Vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Utendaji wa awali wa Mwanafunzi | Utendaji wa wastani wa Mwanafunzi | Utendaji mzuri wa Mwanafunzi | Utendaji mzuri sana wa Mwanafunzi | |
| | | e) Kuelezea vitu vilivyopo katika mazingira yao katika hali ya umoja na wingi kwa (vitu vyenye uhai na visivyo na uhai) | Vitu vyenye uhai na visivyo na uhai vilivyopo katika mazingira yao katika hali ya umoja na wingi vimeelezewa kwa usahihi | Anaelezea vitu katika hali ya umoja na wingi kwa uchache sana | Anaelezea vitu katika hali ya umoja na wingi kwa uchache | Anaelezea vitu vingi katika hali umoja na wingi | Anaelezea vitu vingi sana katika hali ya umoja na wingi kwa usahihi na kutoa mifano | |
| | | f) Kutambua methali zinavyotumika katika mazungumzo na kuelezea maana zake | Methali zinatambuliwa katika mazungumzo na kueleza maana zake kwa usahihi | Anatambua methali chache sana katika mazungumzo na kueleza maana zake kwa kubahatisha | Anatambua methali chache katika mazungumzo na kueleza maana zake | Anatambua methali nyingi katika mazungumzo na kueleza maana zake | Anatambua methali nyingi sana katika mazungumzo na kueleza maana zake kwa kutoa mifano | |
| | | g) Kutumia nahau katika sentensi mbalimbali | Nahau zinatumika katika sentensi kwa usahihi | Anatumia nahau chache sana katika sentensi | Anatumia nahau chache katika sentensi | Anatumia nahau nyingi katika sentensi | Anatumia nahau nyingi sana katika sentensi na kufafanua maana zake | |

| *Umahiri Mkuu* | *Umahiri Mahususi* | *Shughuli za Kutendwa na Mwanafunzi* | *Vigezo vya Upimaji* | *Upimaji wa Viwango vya Utendaji* | | | | *Idadi ya Vipindi* |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | *Utendaji wa awali wa Mwanafunzi* | *Utendaji wa wastani wa Mwanafunzi* | *Utendaji mzuri wa Mwanafunzi* | *Utendaji mzuri sana wa Mwanafunzi* | |
| | | d)Kusimulia hadithi kwa kuzingatia mtiririko wa mawazo | Hadithi inasimuliwa kwa kuzingatia mtiririko wa mawazo kwa ufasaha | Anasimulia hadithi bila mtiririko wa mawazo | Anasimulia hadithi kwa mtiririko usio sahihi | Anasimulia hadithi kwa mtiririko sahihi wa mawazo | Anasimulia hadithi vizuri sana na kuelezea mafunzo yaliyomo. | |
| | | e)Kutoa taarifa kwa ukamilifu kuhusu tukio lililotokea | Taarifa juu ya tukio lililotokea inatolewa kwa mpangilio na kwa ukamilifu | Anatoa taarifa juu ya tukio lililotokea bila mpangilio | Anatoa taarifa juu ya tukio lilillotokea kwa mpangilio | Anatoa taarifa juu ya tukio lililotokea kwa mpangilio unaoeleweka | Anatoa taarifa juu ya tukio lililotokea kwa mpangilio na kwa kufafanua vizuri | |
| | 1.4 Kutumia msamiati katika kuanzisha na kuendeleza mazungumzo katika miktadha mbalimbali | a)Kutaja majina ya wanafamilia nyumbani katika kusimulia hadithi fupi na kubainisha uhusiano wao | Majina ya wanafamilia nyumbani yanaorodheshwa katika usimuliaji wa hadithi na uhusiano wao unabainishwa kwa usahihi | Anataja majina machache sana ya wanafamilia katika kusimulia hadithi bila kubainisha uhusiano | Anataja majina machache ya wanafamilia katika kusimulia hadithi na kubainisha uhusiano wao kwa kubahatisha | Anataja majina mengi ya wanafamilia katika kusimulia hadithi na kubainisha uhusiano uliopo | Anataja majina mengi sana ya wanafamilia katika kusimulia hadithi na kubainisha uhusiano wao kwa kufafanua kwa kutoa mifano | 18 |

| *Umahiri Mkuu* | *Umahiri Mahususi* | *Shughuli za Kutendwa na Mwanafunzi* | *Vigezo vya Upimaji* | *Upimaji wa Viwango vya Utendaji* | | | | *Idadi ya Vipindi* |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | *Utendaji wa awali wa Mwanafunzi* | *Utendaji wa wastani wa Mwanafunzi* | *Utendaji mzuri wa Mwanafunzi* | *Utendaji mzuri sana wa Mwanafunzi* | |
| | | b) Kubainisha majina ya wanyama, muonekano, sauti zao na kueleza wanakoishi | Majina ya wanyama yanabainishwa kwa kuiga sauti zao, na kuelezea mwonekano wao na wanakoishi kwa usahihi | Anabainisha majina machache sana ya wanyama kwa kuiga sauti zao na kushindwa kuelezea muonekano wao na wanakoishi | Anabainisha majina machache ya wanyama, kwa kuiga sauti zao na kuelezea muonekano wao na wanakoishi kwa kubahatisha | Anabainisha majina mengi ya wanyama, kwa kuiga sauti zao na kuelezea mwonekano wao | Anabainisha majina mengi sana ya wanyama kwa kuiga sauti zao na kuelezea mwonekano wao na wanakoishi kwa kutoa mifano | |
| | 1.5 Kutumia maandishi katika kuwasiliana kulingana na miktadha mbalimbali | a) Kuandika kifungu linganifu cha habari kwa kunakili na imla | Kifungu linganifu cha habari kinaandikwa kwa kunakili na imla kwa usahihi | Anaandika kifungu linganifu cha habari kwa kunakili bila kuzingatia alama za uandishi. | Anaandika kifungu cha habari kwa kunakili imla kwa kuzingatia alama za uandishi | Anaandika kifungu linganifu cha habari kwa kunakili na kwa imla kwa kuzingatia alama nyingi za uandishi | Anaandika kifungu linganifu cha habari kwa kunakili na kwa imla kwa kuzingatia alama zote za uandishi. | 50 |

| *Umahiri Mkuu* | *Umahiri Mahususi* | *Shughuli za Kutendwa na Mwanafunzi* | *Vigezo vya Upimaji* | *Upimaji wa Viwango vya Utendaji* | | | | *Idadi ya Vipindi* |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | *Utendaji wa awali wa Mwanafunzi* | *Utendaji wa wastani wa Mwanafunzi* | *Utendaji mzuri wa Mwanafunzi* | *Utendaji mzuri sana wa Mwanafunzi* | |
| | | b) Kuandika sentensi zenye maneno yanayojumuisha herufi mwambatano (**sh, ny, ng, nd, th, mb, kw, dh, th, ng, mbw, ng, chw, ndw, gh, py, nz, ky, lw, pw, sw, tw**) kwa kunakili na kwa imla | Sentensi zenye maneno yanayojumuisha herufi mwambatano (**sh, ny, ng, nd, th, mb, kw**) zinaandikwa kwa kunakili na kwa imla kwa usahihi | Anaandika sen-tensi chache sana zenye maneno yenye herufi mwambatano kwa kunakili na kwa imla | Anaandika sentensi chache zenye maneno yenye herufi mwambatano kwa kunakili na kwa imla | Anaandika sentensi nyingi zenye maneno yenye herufi mwambatano kwa kunakili na kwa imla | Anaandika sentensi nyingi sana zenye maneno yenye herufi mwambatano zote kwa kunakili na kwa imla na kuzingatia alama za uandishi | |
| | | c) Kuandika kwa kuungan-isha sehemu mbili za sentensi ili kupata maana kamili | Sehemu mbili za sentensi zinaandikwa kwa kuunganisha ili kupata maana kamili | Anaandika sentensi chache sana kwa kuunganisha sehemu mbili za sentensi | Anaandika sentensi chache kwa kuunganisha sehemu mbili za sentensi | Anaandika sen-tensi nyingi kwa kuunganisha sehemu mbili za sentensi | Anaandika sentensi nyingi sana kwa kuunganisha sehemu mbili za sentensi na kuzingatia alama za uandishi | |

| *Umahiri Mkuu* | *Umahiri Mahususi* | *Shughuli za Kutendwa na Mwanafunzi* | *Vigezo vya Upimaji* | *Upimaji wa Viwango vya Utendaji* | | | | *Idadi ya Vipindi* |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | *Utendaji wa awali wa Mwanafunzi* | *Utendaji wa wastani wa Mwanafunzi* | *Utendaji mzuri wa Mwanafunzi* | *Utendaji mzuri sana wa Mwanafunzi* | |
| | | d) Kuandika sentensi sahihi kutokana na vifungu vya maneno yaliyo-changanywa | Sentensi sahihi zinaandikwa kutokana na vifungu vya maneno yaliyo-changanywa kwa usahihi | Anaandika sentensi chache sana kutokana na vifungu vya maneno yaliyochanganywa | Anaandika sentensi chache kutokana na vifungu vya maneno yaliyochanganywa | Anaandika sentensi nyingi kutokana na vifungu vya maneno yaliyo-changanywa kwa usahihi | Anaandika sentensi nyingi sana kutokana na vifungu vya maneno yaliyo-changanywa na kuunda habari fupi. | |
| | | e) Kutunga sentensi kwa kutumia maneno teule | Sentensi zinatungwa kwa kutumia maneno teule kwa usahihi. | Anatunga sentensi chache sana kwa kutumia maneno teule na kushind-wa kuziandika | Anatunga sentensi chache kwa kutumia maneno moja teule na kuziandika | Anatunga sen-tensi nyingi kwa kutumia maneno teule na kuzian-dika | Anatunga sen-tensi nyingi sana kwa kutumia maneno teule na kuandika habari fupi. | |
| | | f) Kuandika neno au maneno yaliyokosekana katika sentensi ili kukamilisha maana | Neno au maneno yaliyokosekana katika sentensi yanaandikwa kwa usahihi | Anaandika maneno machache sana yaliyokosekana katika sentensi chache kwa kubahatisha | Anaandika maneno machache yaliyokosekana katika sentensi chache | Anaandika maneno mengi yaliyokosekana katika sentensi nyingi | Anaandika maneno mengi sana yaliyokosekana katika sentensi nyingi | |

| *Umahiri Mkuu* | *Umahiri Mahususi* | *Shughuli za Kutendwa na Mwanafunzi* | *Vigezo vya Upimaji* | *Upimaji wa Viwango vya Utendaji* | | | | *Idadi ya Vipindi* |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | *Utendaji wa awali wa Mwanafunzi* | *Utendaji wa wastani wa Mwanafunzi* | *Utendaji mzuri wa Mwanafunzi* | *Utendaji mzuri sana wa Mwanafunzi* | |
| | | g) Kutunga sentensi zenye maneno yasiyozidi sita zenye kueleweka na ushikamani kwa kuandika | Sentensi zenye maneno yasiyozidi sita zenye kueleweka na ushikamani zinatungwa na kuandikwa kwa usahihi | Anatunga sentensi chache sana zisizo na ushikamani | Anatunga na kuandika sentensi chache zenye kueleweka na ushikamani | Anatunga na kuandika sentensi nyingi zenye kueleweka na ushikamani | Anatunga na kuandika sentensi nyingi sana zenye kueleweka na ushikamani na kuunda habari. | |
| | | h) Kuandika habari kwa kuzingatia kanuni na alama za uandishi | Habari inaandikwa kwa kuzingatia kanuni na alama za uandishi | Anaandika habari kwa kuzingatia kanuni na alama chache sana za uandishi | Anaandika habari kwa kuzingatia kanuni na alama chache za uandishi | Anaandika habari kwa kuzingatia kanuni na alama nyingi za uandishi | Anaandika habari kwa kuzingatia kanuni na alama zote za uandishi | |
| | | i) Kubainisha majina ya wanyama, muonekano, sauti zao na kueleza wanakoishi | Majina ya wanyama yanabainishwa kwa kuiga sauti zao, na kuelezea mwonekano wao na wanakoishi kwa usahihi | Anabainisha majina machache sana ya wanyama kwa kuiga sauti zao na kushindwa kuelezea muonekano wao na wanakoishi | Anabainisha majina machache ya wanyama, kwa kuiga sauti zao na kuelezea muonekano wao na wanakoishi kwa kubahatisha | Anabainisha majina mengi ya wanyama, kwa kuiga sauti zao na kuelezea mwonekano wao | Anabainisha majina mengi sana ya wanyama kwa kuiga sauti zao na kuelezea mwonekano wao na wanakoishi kwa kutoa mifano | |

| Umahiri Mkuu | Umahiri Mahususi | Shughuli za Kutendwa na Mwanafunzi | Vigezo vya Upimaji | Upimaji wa Viwango vya Utendaji | | | | Idadi ya Vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Utendaji wa awali wa Mwanafunzi | Utendaji wa wastani wa Mwanafunzi | Utendaji mzuri wa Mwanafunzi | Utendaji mzuri sana wa Mwanafunzi | |
| | | j) Kuandika sentensi kwa kutumia nyakati mbalimbali (uliopo, ujao uliopita na timilifu) | Sentensi zinaandikwa kwa kutumia nyakati mbalimbali kwa usahihi | Anaandika sentensi chache sana katika nyakati mbalimbali kwa kubahatisha. | Anaandika sentensi chache katika nyakati mbalimbali. | Anaandika sentensi nyingi katika nyakati mbalimbali. | Anaandika sentensi nyingi katika nyakati mbalimbali na kuunda aya. | |
| | 1.6 Kutumia msamiati katika uandishi wa matini mbalim-bali | a) Kuandika habari fupi kwa mpangilio unaoeleweka kuhusu shughuli za kila siku. | Habari fupi inaandikwa kwa mpangilio unaoeleweka kuhusu shughuli za kila siku | Anaandika habari fupi kuhusu shughuli za kila siku bila mpangilio | Anaandika habari fupi kuhusu shughuli za kila siku kwa mpangilio unaoeleweka kwa baadhi ya aya | Anaandika habari fupi kuhusu shughuli za kila siku za mwanafunzi kwa mpangilio | Anaandika habari fupi kuhusu shughuli za kila siku kwa mpangilio unaoeleweka na kwa kuzingatia alama za uandishi. | 10 |
| | | b) Kuandika hadithi fupi kwa kuzingatia kanuni na alama za uandishi | Hadithi fupi inandikwa kwa kuzingatia kanuni na alama za uandishi | Anaandika hadithi fupi kwa kuzingatia kanuni na alama chache sana za uandishi | Anaandika hadithi fupi kwa kuzingatia kanuni na alama chache za uandishi | Anaandika hadithi fupi kwa kuzingatia kanuni na alama nyingi za uandishi | Anaandika hadithi fupi kwa kuzingatia kanuni na alama zote za uandishi | |

| *Umahiri Mkuu* | *Umahiri Mahususi* | *Shughuli za Kutendwa na Mwanafunzi* | *Vigezo vya Upimaji* | *Upimaji wa Viwango vya Utendaji* | | | | *Idadi ya Vipindi* |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | *Utendaji wa awali wa Mwanafunzi* | *Utendaji wa wastani wa Mwanafunzi* | *Utendaji mzuri wa Mwanafunzi* | *Utendaji mzuri sana wa Mwanafunzi* | |
| 2.0 Kuonesha uelewa wa jambo alilo-lisikiliza au kulisoma | 2.1 Kusikiliza na kuonesha uelewa juu ya jambo alilolisikiliza | a) Kutegua na kutega vitendawili | Vitendawili vinategwa na kuteguliwa kwa usahihi | Anatega na kutegua vitendawili vichache sana | Anatega na kutegua vitendawili vichache | Anatega na kutegua vitendawili vingi | Anatega na kutegua vitendawili vingi na kuvifafanua kwa kutoa mifano | 20 |
| | | b) Kutafsiri ujumbe ulio katika methali kwa usahihi | Ujumbe ulio katika methali unatafsiriwa kwa usahihi | Anatafsiri ujumbe ulio katika methali chache sana kwa kubahatisha | Anatafsiri ujumbe ulio katika methali chache | Anatafsiri ujumbe ulio katika methali nyingi | Anatafsiri na kufafanua ujumbe ulio katika methali nyingi sana | |
| | | c) Kutafsiri maana ya nahau iliyotumika katika habari | Maana ya nahau inatafsiriwa kama ilivyotumika katika habari kwa usahihi | Anatafsiri kwa kubahatisha maana ya nahau katika habari. | Anatafsiri maana ya nahau chache katika habari | Anatafsiri maana za nahau nyingi katika habari | Anatafsiri na kufafanua kwa kutoa mifano maana za nahau nyingi katika habari | |
| | | d) Kuonesha hisia za mwili kutokana na kinachozungu-mzwa (Huzuni, furaha, mshtuko na mshangao) | Hisia za mwili zinaoneshwa wazi katika mazungumzo | Anaonesha hisia chache sana za mwili katika mazungumzo | Anaonesha hisia chache za mwili katika mazungumzo | Anaonesha hisia nyingi za mwili katika mazungumzo | Anaonesha kwa vitendo hisia nyingi za mwili katika mazungumzo | |

| *Umahiri Mkuu* | *Umahiri Mahususi* | *Shughuli za Kutendwa na Mwanafunzi* | *Vigezo vya Upimaji* | *Upimaji wa Viwango vya Utendaji* | | | | *Idadi ya Vipindi* |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | *Utendaji wa awali wa Mwanafunzi* | *Utendaji wa wastani wa Mwanafunzi* | *Utendaji mzuri wa Mwanafunzi* | *Utendaji mzuri sana wa Mwanafunzi* | |
| | 2.2 Kusoma kwa ufasaha na kuonesha uelewa wa matini aliyoisoma | a) Kubaini maneno mapya yaliyotumika katika hadithi iliyosomwa na kuyatolea maana | Maneno mapya yaliyotumika katika hadithi iliyosomwa yanabainishwa na kutolewa maana kwa usahihi | Anabainisha maneno mapya machache sana yaliyotumika katika hadithi iliyosomwa na kuyatolea maana | Anabainisha maneno mapya machache yaliyotumika katika hadithi iliyosomwa na kuyatolea maana | Anabainisha maneno mapya mengi yaliyotumika katika hadithi iliyosomwa na kuyatolea maana | Anabainisha maneno mapya mengi sana yaliyotumika katika hadithi iliyosomwa na kuyatolea maana kwa kutoa mifano | 35 |
| | | b) Kueleza sifa na tabia mbalimbali za wadudu | Sifa na tabia mbalimbali za wadudu zimeelezwa kwa usahihi | Anaeleza sifa na tabia chache sana za wadudu | Anaeleza sifa na tabia chache za wadudu | Anaeleza sifa na tabia nyingi za wadudu | Anaeleza sifa na tabia nyingi za wadudu kwa kutoa mifano | |
| | | c) Kusoma kimya kifungu cha habari na kubaini hoja kuu | Kifungu cha habari kimesomwa kimya na kubaini hoja kuu kwa usahihi | Anasoma kimya kifungu cha habari na kubainisha hoja kuu kwa kubahatisha | Anasoma kimya kifungu cha habari na kubaini baadhi ya hoja kuu | Anasoma kimya kifungu cha habari na kubaini hoja kuu nyingi | Anasoma kimya kifungu cha habari na kubaini hoja kuu na kuzifafanua | |

| *Umahiri Mkuu* | *Umahiri Mahususi* | *Shughuli za Kutendwa na Mwanafunzi* | *Vigezo vya Upimaji* | *Upimaji wa Viwango vya Utendaji* | | | | *Idadi ya Vipindi* |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | *Utendaji wa awali wa Mwanafunzi* | *Utendaji wa wastani wa Mwanafunzi* | *Utendaji mzuri wa Mwanafunzi* | *Utendaji mzuri sana wa Mwanafunzi* | |
| | | d) Kusoma kimya kifungu cha habari na kubaini hoja kuu | Kifungu cha habari kinasomwa kimya na kubaini hoja kuu | Anasoma kimya kifungu cha habari na kubaini hoja kuu kwa kukosea | Anasoma kimya kifungu cha habari na kubaini hoja kuu kwa kukosea kidogo | Anasoma kimya kifungu cha habari na kubaini hoja kuu bila kukosea | Anasoma kimya kifungu cha habari na kubaini hoja kuu zote kwa usahihi kama ilivyoku-sudiwa | |
| | | e) Kusoma kwa sauti kifungu cha habari kwa kuzingatia alama za uandishi mkato ( , ) nukta ( .) mshangao (!) kuuliza (?) fungua na funga semi (“”) | Kifungu cha habari kinasomwa kwa sauti kwa kuzingatia alama za uandishi | Anasoma kwa sauti kifungu cha habari kwa kuzingatia alama chache sana za uandishi | Anasoma kwa sauti kifungu cha habari kwa kuzingatia alama chache za uandishi | Anasoma kwa sauti kifungu cha habari kwa kuzingatia alama nyingi za uandishi | Anasoma kwa sauti kifungu cha habari kwa hisia na kwa kuzingatia alama zote za uandishi | |
| | | f) Kubaini nahau na kuelezea maana zake katika matini | Nahau zilizojitokeza katika matini zinabainishwa na kuelezewa maana zake kwa usahihi | Anasoma matini na kubainisha nahau chache sana na kuelezea maana zake | Anasoma matini na kubainisha nahau chache na kuelezea maana zake | Anasoma matini na kubainisha nahau nyingi na kuelezea maana zake | Anasoma matini na kubainisha nahau, kuelezea na kufafanua maana zake | |

| *Umahiri Mkuu* | *Umahiri Mahususi* | *Shughuli za Kutendwa na Mwanafunzi* | *Vigezo vya Upimaji* | *Upimaji wa Viwango vya Utendaji* | | | | *Idadi ya Vipindi* |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | *Utendaji wa awali wa Mwanafunzi* | *Utendaji wa wastani wa Mwanafunzi* | *Utendaji mzuri wa Mwanafunzi* | *Utendaji mzuri sana wa Mwanafunzi* | |
| | | g) Kusoma shairi kishairi | Shairi linasomwa kwa sauti ya kishairi kwa ufasaha. | Anasoma shairi na kuzingatia sauti ya kishairi katika beti chache sana | Anasoma shairi kwa kuzingatia sauti ya shairi katika beti chache | Anasoma shairi kwa kuzingatia sauti ya kishairi katika beti nyingi | Anasoma shairi kwa sauti ya kishairi katika beti zote za shairi | |
| | 2.3 Kutumia msamia-ti katika kusoma ili kuchan-ganua mawazo yaliyo was-ilishwa ka-tika matini mbalimbali | a) Kubaini maneno mapya kutoka kwenye kifungu cha habari na kuelezea maana zake | Maneno mapya yanabainishwa kutoka kwenye kifungu cha habari na maana zake zinaelezewa kwa usahihi. | Anabainisha maneno mapya machache sana kutoka kwenye kifungu cha habari na kuelezea maana zake | Anabainisha maneno mapya machache kutoka kwenye kifungu cha habari na kuelezea maana zake | Anabainisha maneno mapya mengi kutoka kwenye kifungu cha habari na kuelezea maana zake | Anabainisha maneno mapya mengi kutoka kwenye kifungu cha habari na kuelezea maana zake kwa kutoa mifano. | 15 |
| | | b) Kutambua maneno yenye maana sawa (visawe) kwa kutumia kamusi | Maneno yenye maana sawa yanatambuliwa kwa kutumia kamusi | Anatambua maneno machache sana yenye maana sawa | Anatambua maneno machache yenye maana sawa | Anatambua maneno mengi yenye maana sawa kwa kutumia kamusi | Anatambua maneno yenye maana sawa kwa kutumia kamusi na kuyatungia sentensi | |
| | | c) Kutumia kamusi ili kueleza maana za maneno yaliyotumika katika habari | Maana za maneno yaliyotumika katika habari zinaelezewa kwa usahihi | Anaeleza maana za maneno machache sana yaliyotumika katika habari | Anaeleza maana za maneno machache yaliyotumika katika habari | Anaeleza maana ya maneno mengi yaliyotumika katika habari | Anaeleza na kufafanua maana za maneno mengi sana yaliyotumika katika habari | |

### 3.8 Maudhui ya Darasa la IV

Umahiri Utakaojengwa na Mwanafunzi katika Somo

| | Umahiri mkuu | Umahiri mahususi |
|---|---|---|
| 1. | Kuwasiliana katika miktadha mbalimbali | 1.1 Kuanzisha na kuendeleza mazungumzo katika miktadha mbalimbali.<br>1.2 Kutumia maandishi katika mawasiliano kulingana na miktadha mbalimbali. |
| 2. | Kuonesha uelewa wa jambo alilolisikiliza au kulisoma | 2.1 Kusikiliza na kuonesha uelewa wa jambo alilolisikiliza.<br>2.2 Kusoma kwa ufasaha na kuonesha uelewa wa matini aliyoisoma. |
| 3. | Kutumia msamiati katika miktadha mbalimbali | 3.1 Kuzungumza kwa kuwasilisha hoja kulingana na miktadha mbalimbali.<br>3.2 Kutumia maandishi katika kuandaa matini mbalimbali.<br>3.3 Kusoma na kuchanganua mawazo yaliyowasilishwa katika matini mbalimbali. |

**Angalizo:** Katika jedwali la maudhui ya muhtasari katika kurasa zinazofuata umahiri huo mkuu wa kutumia msamiati katika miktadha mbalimbali hautasimama peke yake kama umahiri mkuu. Hivyo utajitokeza kama umahiri mahususi unaoingiliana na kila umahiri mahususi ndani ya umahiri mkuu wa kuwasiliana katika miktadha mbalimbali na umahiri mkuu wa kusoma kwa ufahamu katika kujenga uwezo wa kujieleza kwa namna mbalimbali.

## Jedwali la Maudhui ya Muhtasari

| *Umahiri Mkuu* | *Umahiri Mahususi* | *Shughuli za Kutendwa na Mwanafunzi* | *Vigezo vya Upimaji* | *Upimaji wa Viwango vya Utendaji* | | | | *Idadi ya Vipindi* |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | *Utendaji wa awali wa Mwanafunzi* | *Utendaji wa wastani wa Mwanafunzi* | *Utendaji mzuri wa Mwanafunzi* | *Utendaji mzuri sana wa Mwanafunzi* | |
| 1. Kuwasiliana katika miktadha mbalimbali | 1.1 Kuanzisha na kuendeleza mazungumzo katika miktadha mbalimbali | a) Kutaja neno moja lililobeba maana ya jumla badala ya kifungu cha maneno (kuku, njiwa, kunguru - ndege) | Neno moja lililobeba maana ya jumla badala ya kifungu cha maneno linatajwa kwa usahihi | Anataja kifungu cha maneno badala ya neno moja la jumla | Anataja maneno mengi badala ya kutaja neno moja la jumla | Anataja neno moja linalobeba maana ya jumla katika kifungu cha maneno | Anataja neno moja la jumla linalobeba maana badala ya kifungu cha maneno kwa kufafanua | 47 |
| | | b) Kutega na kutegua vitendawili vinavyoakisiwa na picha | Vitendawili vinavyoakisiwa na picha vinategwa na kuteguliwa kwa usahihi | Anatega na kutegua vitendawili vichache sana vinavyoakisiwa na picha. | Anatega na kutegua vitendawili vichache vinavyoakisiwa na picha | Anatega na kutegua vitendawili vingi vinavyo akisiwa na picha | Anatega na kutegua vitendawili vingi sana vinavyoakisiwa na picha na kuvihusianisha na vitu vilivyo katika mazingira. | |
| | | c) Kufafanua ujumbe uliomo kwenye methali zilizotolewa | Ujumbe uliomo kwenye methali zilizotolewa unafafanuliwa kwa usahihi | Anafafanua ujumbe uliomo katika methali chache sana | Anafafanua ujumbe uliomo katika methali chache kwa | Anafafanua ujumbe uliomo katika methali nyingi | Anafafanua na kuelezea ujumbe uliomo katika methali nyingi kwa kutoa mifano | |
| | | d) Kueleza maana zilizomo kwenye nahau zilizo orodheshwa | Maana zilizomo katika nahau zinaorodheshwa na kuelezewa kwa usahihi | Anaelezea maana zilizomo katika nahau chache sana | Anaelezea maana zilizomo katika nahau chache | Anaelezea maana zilizomo katika nahau nyingi kwa usahihi | Anaelezea na kufafanua maana zilizomo katika nahau nyingi zilizo orodheshwa. | |

| *Umahiri Mkuu* | *Umahiri Mahususi* | *Shughuli za Kutendwa na Mwanafunzi* | *Vigezo vya Upimaji* | *Upimaji wa Viwango vya Utendaji* | | | | *Idadi ya Vipindi* |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | *Utendaji wa awali wa Mwanafunzi* | *Utendaji wa wastani wa Mwanafunzi* | *Utendaji mzuri wa Mwanafunzi* | *Utendaji mzuri sana wa Mwanafunzi* | |
| | | e) Kulinganisha vitu kwa kuzingatia ukubwa na udogo kwa kutumia muundo teule | Vitu vinalinganishwa kwa kuzingatia ukubwa na udogo kwa kutumia muundo teule kwa usahihi | Analinganisha vitu ambavyo havilingani kwa ukubwa na udogo wake kwa kutumia muundo teule | Analinganisha vitu vichache bila kutofautisha ukubwa na udogo kwa kutumia muundo teule | Analinganisha vitu vingi kwa kutofautisha ukubwa na udogo kwa kutumia muundo teule. | Analinganisha, anatofautisha na kuelezea vitu vingi sana kwa ukubwa na udogo wake kwa kutumia muundo teule | |
| | | f) Kutambua na kuelezea rangi za vitu mbalimbali | Rangi za vitu mbalimbali zinatambuliwa na kuelezewa kwa usahihi | Anatambua rangi za vitu vichache sana na kuzielezea | Anatambua rangi za vitu vichache na kuzielezea. | Anatambua rangi za vitu vingi na kuzielezea kwa usahihi | Anatambua rangi za vitu vingi sana na kuzifafanua | |
| | | g) Kuelezea watu kwa kuzingatia shughuli zao | Watu wanaelezewa kwa kuzingatia shughuli zao kwa usahihi | Anaelezea watu wachache sana kwa kuzingatia shughuli zao | Anaelezea watu wachache kwa kuzingatia shughuli | Anaelezea watu wengi kwa kuzingatia shughuli zao. | Anaelezea watu wengi sana kwa kuzingatia shughuli zao kwa kutoa mifano | |
| | | h) Kueleza matukio kwa kutumia nyakati mbalimbali katika sentensi<br>- Uliopo<br>- uliopita<br>- ujao<br>- timilifu | Matukio yanaelezwa katika sentensi kwa kutumia nyakati mbalimbali kwa usahihi | Anaelezea matukio katika sentensi chache sana kwa kutumia wakati uliopo, uliopita, ujao na timilifu kwa kubahatisha | Anaelezea matukio katika sentensi chache kwa kutumia wakati uliopo, uliopita, ujao na timilifu | Anaelezea matukio katika sentensi nyingi kwa kutumia wakati uliopo, uliopita, ujao na timilifu. | Anaelezea matukio katika sentensi nyingi sana kwa kutumia nyakati zote (uliopita, uliopo, timilifu, na ujao kwa hisia) | |

| *Umahiri Mkuu* | *Umahiri Mahususi* | *Shughuli za Kutendwa na Mwanafunzi* | *Vigezo vya Upimaji* | *Upimaji wa Viwango vya Utendaji* | | | | *Idadi ya Vipindi* |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | *Utendaji wa awali wa Mwa-nafunzi* | *Utendaji wa wastani wa Mwanafunzi* | *Utendaji mzuri wa Mwanafunzi* | *Utendaji mzuri sana wa Mwanafunzi* | |
| | | i) Kukanusha matukio ya nyakati mbalimbali katika sentensi | Matukio ya nyakati mbalimbali yanakanushwa katika sentensi kwa usahihi | Anakanusha matukio ya nyakati chache sana katika sentensi kwa kubahatisha | Anakanusha matukio ya nyakati chache katika sentensi | Anakanusha matukio ya nyakati nyingi katika sentensi | Anakanusha matukio ya nyakati zote katika sentensi nyingi na kutoa ufafanuzi | |
| | | j) Kuonesha hali ya hisia katika mazungumzo (furaha, huzuni, mshangao, mshtuko) | Hali ya hisia inaoneshwa katika mazungumzo kwa usahihi | Anaonesha hali ya hisia ya mshangao katika mazungumzo | Anaonesha hali ya hisia ya mshangao na huzuni katika mazungumzo | Anaonesha hali ya hisia ya mshangao, huzuni na furaha katika mazungumzo | Anaonesha kwa vitendo hali ya hisia zote furaha, huzuni, mshangao na mshtuko katika mazungumzo | |
| | | k) Kutoa maelekezo yanayoeleweka na kutekelezwa na wenzake. | Maelekezo yanayoeleweka yanatolewa na kutekelezwa na wenzake kwa usahihi | Anatoa maelekezo yasiyoeleweka kwa wenzake | Anatoa maelekezo yasiyojitosheleza kwa wenzake | Anatoa maelekezo yanayoeleweka vizuri na kutekelezeka kwa wenzake | Anatoa maelekezo yanayoeleweka vizuri sana kwa kutoa mifano na kutekelezeka kwa wenzake. | |

| *Umahiri Mkuu* | *Umahiri Mahususi* | *Shughuli za Kutendwa na Mwanafunzi* | *Vigezo vya Upimaji* | *Upimaji wa Viwango vya Utendaji* | | | | *Idadi ya Vipindi* |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | *Utendaji wa awali wa Mwanafunzi* | *Utendaji wa wastani wa Mwanafunzi* | *Utendaji mzuri wa Mwanafunzi* | *Utendaji mzuri sana wa Mwanafunzi* | |
| | 1.2 Kutumia msamiati katika kuzungumza kwa kuwasilisha hoja kulingana na muktadha mbalimbali | a) Kutaja majina ya mavazi ya wanaume na wanawake na kuyaelezea | Majina ya mavazi ya wanaume na wanawake yanatajwa na kuelezewa kwa ufasaha | Anataja majina machache sana ya mavazi ya wanawake na wanaume na kuyaelezea kwa kubahatisha | Anataja majina machache ya mavazi ya wanawake na wanaume na kuyaelezea kwa kuchanganya | Anataja majina mengi ya mavazi ya wanawake na wanaume na kuyaelezea | Anataja na kuelezea kwa ufasaha majina yote ya mavazi ya wanawake na wanaume kwa kutoa mifano | 26 |
| | | b) Kujadili majina ya vinywaji na kuelezea faida na hasara zake kwa watumiaji | Majina ya vinywaji yanajadiliwa na kuelezewa faida na hasara zake kwa watumiaji kwa usahihi | Anashiriki katika kujadili majina ya vinywaji vichache sana bila kuelezea faida na hasara zake | Anashiriki katika kujadili majina ya vinywaji vichache na kuelezea faida bila hasara zake | Ashiriki katika kujadili majina ya vinywaji vingi na kuelezea faida na hasara zake | Anashiriki katika kujadili majina ya vinywaji vingi sana na kuelezea faida na hasara zake kwa kutoa mifano | |
| | | c) Kubainisha majina ya mimea iliyo katika mazingira yao na kuelezea umuhimu wake kwa binadamu | Majina ya mimea iliyo katika mazingira yao yanabainishwa na kuelezewa umuhimu wake kwa binadamu kwa ufasaha | Anabainisha majina machache sana ya mimea bila kueleza umuhimu wake kwa binadamu | Anabainisha majina machache ya mimea na kueleza umuhimu wake kwa binadamu | Anabainisha majina mengi ya mimea na anaweza kuelezea umuhimu wake kwa binadamu | Anabainisha majina mengi sana ya mimea na anaweza kuelezea umuhimu wake kwa binadamu kwa kutoa mifano | |

| *Umahiri Mkuu* | *Umahiri Mahususi* | *Shughuli za Kutendwa na Mwanafunzi* | *Vigezo vya Upimaji* | *Upimaji wa Viwango vya Utendaji* | | | | *Idadi ya Vipindi* |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | *Utendaji wa awali wa Mwanafunzi* | *Utendaji wa wastani wa Mwanafunzi* | *Utendaji mzuri wa Mwanafunzi* | *Utendaji mzuri sana wa Mwanafunzi* | |
| | | d) Kutaja majina ya vifaa vinavyotumika katika zahanati na kuelezea kazi zake. | Majina ya vifaa vinavyotumika katika zahanati yanatajwa na kuelezewa kazi zake | Anataja majina ya vifaa vichache sana vinavyo patikana katika zahanati bila kuelezea kazi zake | Anataja majina ya vifaa vichache vinavyopatikana zahanati na kuelezea kazi zake | Anataja majina ya vifaa vingi vinavyopatikana katika zahanati na kuelezea kazi zake | Anataja majina ya vifaa vingi sana vinavyopatikana katika zahanati na kuelezea kazi zake kwa kutoa mifano | |
| | | e) Kutumia nyakati mbalimbali katika sentensi | Nyakati mbalimbali zimetumika katika sentensi kwa usahihi | Anatumia nyakati chache sana katika sentensi kwa kubahatisha | Anatumia nyakati chache katika sentensi kwa kukosea kidogo | Anatumia nyakati nyingi katika sentensi | Anatumia nyakati zote kikamilifu katika sentensi na kutoa ufafanuzi | |
| | | f) Kuelezea kazi zinazofanyika kila siku kwa kuzingatia wakati uliopo, ujao na uliopita | Kazi zinazofanyika kila siku zinaelezewa kwa kuzingatia nyakati kwa usahihi. | Anaelezea kazi chache sana zinazofanyika kila siku kwa kuzingatia wakati uliopo. | Anaelezea kazi chache zinazofanyika kila siku kwa kuzingatia wakati uliopo na ujao tu. | Anaelezea kazi nyingi zinazofanyika kila siku kwa kuzingatia wakati uliopo, ujao na uliopita | Anaelezea kikamilifu kazi zote zinazofanyika kila siku kwa kuzingatia wakati uliopo, ujao na uliopita kwa kutoa mifano. | |

| *Umahiri Mkuu* | *Umahiri Mahususi* | *Shughuli za Kutendwa na Mwanafunzi* | *Vigezo vya Upimaji* | *Upimaji wa Viwango vya Utendaji* | | | | *Idadi ya Vipindi* |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | *Utendaji wa awali wa Mwanafunzi* | *Utendaji wa wastani wa Mwanafunzi* | *Utendaji mzuri wa Mwanafunzi* | *Utendaji mzuri sana wa Mwanafunzi* | |
| | 1.3 Kutumia maandishi katika mawasiliano kulingana na miktadha mbalimbali | a) Kuandika sentensi kwa kuzingatia alama za uandishi | Sentensi zinaandikwa kwa kuzingatia alama za uandishi kwa usahihi | Anaandika sentensi kwa kuzingatia alama chache sana za uandishi | Anaandika sentensi kwa kuzingatia alama chache za uandishi | Anaandika sentensi kwa kuzingatia alama nyingi za uandishi | Anaandika sentensi nyingi sana kwa kuzingatia alama zote za uandishi | 30 |
| | | b) Kuandika kifungu cha habari kwa mfuatano wa matukio kwa kuzingatia alama za uandishi | Kifungu cha habari kinaandikwa kwa mfuatano sahihi wa matukio kwa kuzingatia alama za uandishi | Anaandika kifungu cha habari kwa mfuatano sahihi wa matukio bila kuzingatia alama za uandishi | Anaandika kifungu cha habari kwa mfuatano sahihi wa matukio kwa kuzingatia alama chache za uandishi | Anaandika kifungu cha habari kwa mfuatano sahihi wa matukio kwa kuzingatia alama nyingi za uandishi | Anaandika kifungu cha habari kwa mfuatano sahihi wa matukio kwa kuzingatia alama zote za uandishi | |
| | | c) Kuandika sentensi zenye kuonesha mahali watu/ vitu walipo/ vilipo (nyuma ya, ndani ya, katikati ya, nje ya, chini ya, juu ya, pembeni ya, kando ya ) | Sentensi zenye kuonesha mahali watu walipo/ vitu vilipo/ zinaandikwa kwa usahihi | Anaandika sentensi chache sana zenye kuonesha mahali watu/vitu walipo/vilipo | Anaandika sentensi chache zenye kuonesha mahali watu walipo/ vitu vilipo | Anaandika sentensi nyingi zenye kuonesha mahali watu walipo/ vitu vilipo. | Anaandika sentensi nyingi zenye kuonesha mahali watu walipo/ vitu vilipo | |

| Umahiri Mkuu | Umahiri Mahususi | Shughuli za Kutendwa na Mwanafunzi | Vigezo vya Upimaji | Upimaji wa Viwango vya Utendaji | | | | Idadi ya Vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Utendaji wa awali wa Mwanafunzi | Utendaji wa wastani wa Mwanafunzi | Utendaji mzuri wa Mwanafunzi | Utendaji mzuri sana wa Mwanafunzi | |
| | | d) Kuandika kifungu cha habari chenye maneno yasiyozidi sabini kuhusu madawa ya kulevya kwa kuzingatia alama za uandishi | Kifungu cha habari chenye maneno yasiyozidi sabini kuhusu madawa ya kulevya kinaandikwa kwa kuzingatia alama za uandishi kwa usahihi | Anaandika kifungu cha habari chenye maneno yasiyozidi sabini kwa kuzingatia alama ya kituo | Anaandika kifungu cha habari chenye maneno yasiyozidi sabini kwa kuzingatia alama za vituo na mkato | Anaandika kifungu cha habari chenye maneno yasiyozidi sabini na kuzingatia alama za vituo, mkato na mshangao | Anaandika kifungu cha habari chenye maneno yasiyozidi sabini kwa mtiririko wenye mantiki na kwa kuzingatia alama zote za uandishi. | |
| | | e) Kuandika hadithi fupi inayoeleweka kwa kuzingatia alama za uandishi | Hadithi fupi inayoeleweka inaandikwa kwa kuzingatia alama za uandishi kwa usahihi | Anaandika hadithi fupi kwa kuzingatia alama ya kituo | Anaandika hadithi fupi inayoeleweka kwa kuzingatia alama za vituo na mkato | Anaandika hadithi inayoeleweka kwa kuzingatia alama za vituo, mkato na mshangao | Anaandika hadithi inayoeleweka na yenye mtiririko kwa kuzingatia alama zote za uandishi | |
| | | f) Kuandika maelekezo ya jinsi ya kupika chai kwa kuzingatia vifaa vinavyotumika na hatua zake | Maelekezo ya jinsi ya kupika chai kwa kuzingatia vifaa vinavyotumika na hatua zake yanaandikwa kwa ukamilifu | Anaandika maelekezo ya jinsi ya kupika chai kwa kuzingatia baadhi ya hatua na vifaa vinavyotumika. | Anaandika maelekezo jinsi ya kupika chai kwa kuzingatia hatua na vifaa vichache vinavyotumika | Anaandika maelekezo jinsi ya kupika chai kwa kuzingatia hatua na vifaa vyake vinavyotumika kwa mtiririko mzuri | Anaandika maelekezo jinsi ya kupika chai kwa kuzingatia hatua na vifaa vyake vinavyotumika kwa mtiririko mzuri | |

| Umahiri Mkuu | Umahiri Mahususi | Shughuli za Kutendwa na Mwanafunzi | Vigezo vya Upimaji | Upimaji wa Viwango vya Utendaji | | | | Idadi ya Vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Utendaji wa awali wa Mwanafunzi | Utendaji wa wastani wa Mwanafunzi | Utendaji mzuri wa Mwanafunzi | Utendaji mzuri sana wa Mwanafunzi | |
| | | g) Kuandika barua ya kirafiki kwa mpangilio na ukamilifu | Barua ya kirafiki inaandikwa kwa mpangilio na kwa kuzingatia vipengele vyote vya muundo wa barua ya kirafiki. | Anaandika barua ya kirafiki bila kuwa na anuani ya mwandishi na utangulizi wa barua | Anaandika barua ya kirafiki kwa kuonesha anuani ya mwandishi na utangulizi wa barua | Anaandika barua ya kirafiki kwa kuonesha anuani ya mwandishi utangulizi wa barua, kiini na mwisho wa barua | Anaandika barua ya kirafiki kwa mpangilio na kwa kuzingatia anuani ya mwandishi, utangulizi, kiini cha barua, mwisho wa barua, saini na jina la mwandishi | |
| | 1.4 Kutumia msamiati katika maandishi katika kuandaa matini mbalimbali | a) Kutaja majina ya mavazi mbalimbali na kuyaelezea kwa sentensi zinazoeleweka | Majina ya mavazi mbalimbali yanatajwa na kuelezewa kwa umahiri kwa sentensi zinazoeleweka. | Anataja majina mbalimbali ya mavazi ya kike na kuyaelezea kwa kubahatisha | Anataja majina mbalimbali ya mavazi ya kike na kiume na kuyaelezea kwa sentensi zinazoeleweka | Anataja majina mbalimbali ya mavazi ya kike na ya kiume na kuyaelezea kwa sentensi zinazoeleweka na kutoa mifano | Anatumia majina ya mavazi yote katika sentensi, kifungu cha habari na kufafanua kazi zake ipasavyo | 17 |
| | | b) Kuandika hadithi fupi kwa kutumia majina ya ndege | Majina ya ndege yanatumiwa katika hadithi fupi kwa usahihi | Anaandika hadithi fupi kwa kutumia majina machache sana ya ndege | Anaandika hadithi fupi kwa kutumia majina machache ya ndege | Anaandika hadithi fupi kwa kutumia majina mengi ya ndege | Anaandika hadithi fupi kwa kutumia majina mengi sana ya ndege | |
| | | c) Kuandika kifungu cha habari na kubaini maneno mapya | Kifungu cha habari kinaandikwa kwa usahihi na maneno mapya yanabainishwa | Anaandika kifungu cha habari bila kubainisha maneno mapya | Anaandika kifungu cha habari na kubainisha maneno mapya machache | Anaandika kifungu cha habari na kubainisha maneno mapya mengi | Anaandika kifungu cha habari na kubainisha maneno mapya na kuelezea maana zake | |

| Umahiri Mkuu | Umahiri Mahususi | Shughuli za Kutendwa na Mwanafunzi | Vigezo vya Upimaji | Upimaji wa Viwango vya Utendaji | | | | Idadi ya Vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Utendaji wa awali wa Mwanafunzi | Utendaji wa wastani wa Mwanafunzi | Utendaji mzuri wa Mwanafunzi | Utendaji mzuri sana wa Mwanafunzi | |
| | | d) Kuandika majina ya mahali na kuelezea shughuli zinazofanyika mahali hapo | Majina ya mahali yanaandikwa na shughuli zinazofanyika zinaelezwa kwa usahihi | Anaandika majina ya mahali na kuelezea shughuli chache sana | Anaandika majina ya mahali na kuelezea shughuli chache zinazofanyika mahali hapo | Anaandika majina ya mahali na kuelezea shughuli nyingi zinazofanyika mahali hapo | Anaandika majina ya mahali na kuelezea shughuli nyingi zinazofanyika kwa kutoa mifano | |
| 2. Kuonesha uelewa wa jambo alilosikiliza au kulisoma | 2.1 Kusikiliza na kuonesha uelewa wa matini mbalimbali | a) Kusikiliza vitendawili na kuvitegua ili kupata maana | Vitendawili vinateguliwa na kutolewa maana zake kwa usahihi | Anategua vitendawili vichache sana bila kutolea maana | Anategua vitendawili vichache na kutolea maana | Anategua vitendawili vingi na kuvitolea maana | Anategua vitendawili vyote vilivyotegwa na kuvitolea maana na kuelezea umuhimu wake katika maisha. | 39 |
| | | b) Kusikiliza nahau na kuelezea maana zake | Maana za nahau zinaelezwa kwa usahihi | Anaelezea maana za nahau chache sana | Anaelezea maana za nahau chache | Anaelezea maana za nahau nyingi | Anaelezea maana za nahau zote na kutoa mifano | |
| | | c) Kusikiliza hadithi na kubaini ujumbe uliopo | Ujumbe uliopo katika hadithi unabainishwa na maana yake zinaelezewa ipasavyo. | Anabainisha ujumbe kidogo sana uliopo katika hadithi kwa kubahatisha | Anabainisha ujumbe kidogo uliopo katika hadithi aliyoisikiliza kwa kusita kidogo | Anabainisha ujumbe uliopo katika hadithi | Anabainisha ujumbe sahihi uliopo katika hadithi na kuelezea maana yake | |

| *Umahiri Mkuu* | *Umahiri Mahususi* | *Shughuli za Kutendwa na Mwanafunzi* | *Vigezo vya Upimaji* | *Upimaji wa Viwango vya Utendaji* | | | | *Idadi ya Vipindi* |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | *Utendaji wa awali wa Mwanafunzi* | *Utendaji wa wastani wa Mwanafunzi* | *Utendaji mzuri wa Mwanafunzi* | *Utendaji mzuri sana wa Mwanafunzi* | |
| | | d) Kusikiliza habari na kubaini ujumbe | Ujumbe uliopo katika habari unabainishwa | Anabainisha sehemu ya ujumbe uliopo katika hadithi | Anabainisha ujumbe kidogo kulingana na habari aliyosikiliza | Anabaini ujumbe uliopo katika habari na kutoa ufafanuzi mfupi | Anabaini ujumbe sahihi uliopo katika habari na kufafanua maana yake | |
| | | e) Kusikiliza mashairi na kubaini ujumbe | Ujumbe unaopatikana katika mashairi unabainishwa ipasavyo | Anabainisha ujumbe kwa kukosea na kuacha mambo mengi | Anabainisha ujumbe usio sahihi kulingana na mashairi aliyo sikiliza | Anabainisha ujumbe katika mashairi na kuelezea maana | Anabainisha ujumbe sahihi ulio katika mashairi kwa kufafanua maana yake kwa ufasaha | |
| | | f) Kusikiliza maelekezo ya uelekeo wa pande za Dunia na kuyatekeleza | Maelekezo ya uelekeo wa pande za dunia yanatekelezwa ipasavyo | Anatekeleza robo ya maelekezo ya uelekeo wa pande za dunia | Anatekeleza nusu ya maelekezo ya uelekeo wa pande za dunia | Anatekeleza robo tatu ya maelekezo ya uelekeo wa pande za dunia | Anatekeleza maelekezo yote ya uelekeo wa pande zote za dunia | |
| | | g) Kusikiliza maelekezo ya uelekeo wa pande mbalimbali na kuyatekeleza (kulia, kushoto, mbele, nyuma, juu, chini) | Maelekezo ya pande mbalimbali za uelekeo yanatekelezwa ipasavyo | Anatekeleza robo ya maelekezo ya uelekeo wa pande anuai | Anatekeleza nusu ya maelekezo ya uelekeo wa pande anuai | Anatekeleza robo tatu ya maelekezo ya uelekeo wa pande anuai | Anatekeleza maelekezo yote ya uelekeo wa pande anuai | |

| *Umahiri Mkuu* | *Umahiri Mahususi* | *Shughuli za Kutendwa na Mwanafunzi* | *Vigezo vya Upimaji* | *Upimaji wa Viwango vya Utendaji* | | | | *Idadi ya Vipindi* |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | *Utendaji wa awali wa Mwanafunzi* | *Utendaji wa wastani wa Mwanafunzi* | *Utendaji mzuri wa Mwanafunzi* | *Utendaji mzuri sana wa Mwanafunzi* | |
| | | h) Kusikiliza maelekezo ya jumla na kuyatekeleza | Maelekezo ya jumla yanasikilizwa na kutekelezwa ipasavyo | Anatekeleza robo ya maelekezo ya jumla | Anatekeleza nusu ya maelekezo ya jumla | Anatekeleza robo tatu ya maelekezo ya jumla | Anatekeleza maelekezo yote ya jumla | |
| | 2.2 Kusoma kwa ufasaha na kuonesha uelewa wa matini aliyoisoma | a) Kusoma kimya matini mbalimbali na kubaini hoja kuu | Matini mbalimbali zinasomwa na hoja kuu zinabainishwa kwa usahihi | Anasoma kimya matini chache sana na kubainisha hoja kuu kwa kukosea | Anasoma kimya matini chache na kubainisha hoja kuu | Anasoma kimya matini nyingi na kubainisha hoja kuu | Anasoma kimya na kuelewa matini nyingi sana na kubainisha hoja kuu zote | 18 |
| | | b) Kusoma hadithi kwa sauti kwa kuzingatia alama za uandishi | Hadithi inasomwa kwa sauti kwa kuzingatia alama za uandishi | Anasoma hadithi kwa sauti na kuzingatia alama chache sana za uandishi | Anasoma hadithi kwa sauti na kuzingatia alama chache za uandishi | Anasoma hadithi kwa sauti na kuzingatia alama nyingi za uandishi | Anasoma hadithi kwa sauti na kuzingatia alama zote za uandishi | |

| *Umahiri Mkuu* | *Umahiri Mahususi* | *Shughuli za Kutendwa na Mwanafunzi* | *Vigezo vya Upimaji* | *Upimaji wa Viwango vya Utendaji* | | | | *Idadi ya Vipindi* |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | *Utendaji wa awali wa Mwanafunzi* | *Utendaji wa wastani wa Mwanafunzi* | *Utendaji mzuri wa Mwanafunzi* | *Utendaji mzuri sana wa Mwanafunzi* | |
| | | c) Kusoma shairi kwa sauti ya kishairi | Shairi linasomwa kishairi kwa ufasaha | Anasoma shairi kwa sauti ya kishairi kwa kukosea | Anasoma beti chache za shairi kwa sauti ya kishairi | Anasoma shairi kwa sauti ya kishairi | Anasoma na kuelewa beti zote za shairi kwa sauti ya kishairi | |
| | | d) Kusoma ngonjera kwa sauti ya kutamba | Ngonjera inasomwa kwa sauti ya kutamba kama ilivyokusudiwa | Anasoma ngonjera bila sauti ya kutamba | Anasoma ngonjera kwa sauti ya kutamba na kusitasita | Anasoma ngonjera kwa sauti ya kutamba | Anasoma ngonjera kwa sauti ya kutamba kama ilivyokusudiwa | |
| | 2.3 Kutumia msamiati katika kuchanganua mawazo yaliyo wasilishwa katika muktadha mbalimbali | a) Kubainisha majina na kuyabadili kuwa matendo (somo-soma kilimo-kulima) | Majina yanabainishwa na kubadilishwa kuwa matendo kwa usahihi | Anabainisha majina machache sana na kubadilisha kuwa matendo | Anabainisha majina machache na kuyabadilisha kuwa matendo | Anabainisha majina mengi na kuyabadilisha kuwa matendo | Anabainisha majina mengi sana na kuyabadilisha kuwa matendo | 18 |

| *Umahiri Mkuu* | *Umahiri Mahususi* | *Shughuli za Kutendwa na Mwanafunzi* | *Vigezo vya Upimaji* | *Upimaji wa Viwango vya Utendaji* | | | | *Idadi ya Vipindi* |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | *Utendaji wa awali wa Mwanafunzi* | *Utendaji wa wastani wa Mwanafunzi* | *Utendaji mzuri wa Mwanafunzi* | *Utendaji mzuri sana wa Mwanafunzi* | |
| | | c) Kuunda maneno mapya kwa kudondosha herufi moja au silabi kutoka kwenye neno (ondoa-ndoa Kamata-kata) | Maneno mapya yanaundwa kwa kudondosha herufi moja au silabi kutoka kwenye neno | Anaunda maneno machache sana kwa kudondosha herufi moja au silabi kutoka kwenye neno | Anaunda maneno machache kwa kudondosha herufi moja au silabi kutoka kwenye neno | Anaunda maneno mengi kwa kudondosha herufi moja au silabi kutoka kwenye neno | Anaunda maneno mengi sana kwa kudondosha herufi moja au silabi kutoka kwenye neno na kuyatungia sentensi | |
| | | d) Kusoma maneno mbalimbali na kubainisha kinyume chake | Maneno mbalimbali yanasomwa kwa ufasaha na kubainisha kinyume chake | Anasoma maneno machache sana na kubainisha kinyume chake | Anasoma maneno machache na kubainisha kinyume chake | Anasoma maneno mengi na kubainisha kinyume chake kwa ufasaha | Anasoma maneno yote kwa ufasaha na kubainisha kinyume chake kisha kuyatungia sentensi | |

### 3.9 Maudhui ya Darasa la V

Umahiri Utakaojengwa na Mwanafunzi katika Somo

| Umahiri Mkuu | Umahiri Mahususi |
|---|---|
| 1. Kuwasiliana katika miktadha mbalimbali. | 1.1 Kuanzisha na kuendeleza mazungumzo katika miktadha mbalimbali.<br>1.2 Kutumia maandishi katika mawasiliano kulingana na miktadha mbalimbali. |
| 2. Kuonesha uelewa wa jambo alilolisikiliza au kulisoma | 2.1 Kusikiliza na kuonesha uelewa wa jambo alilolisikiliza.<br>2.2 Kusoma kwa ufasaha na kuonesha uelewa wa matini aliyoisoma. |
| 3. Kutumia msamiati katika miktadha mbalimbali | 3.1 Kuzungumza kwa kuwasilisha hoja katika miktadha mbalimbali.<br>3.2 Kutumia maandishi katika kuandaa matini mbalimbali.<br>3.3 Kusoma na kuchanganua mawazo yaliyowasilishwa katika matini mbalimbali. |

**Angalizo:** Katika jedwali la maudhui ya muhtasari kwenye kurasa zinazofuata umahiri mkuu wa kutumia msamiati katika miktadha mbalimbali hautasimama peke yake kama umahiri mkuu. Hivyo umahiri huo utajitokeza kama umahiri mahususi unaoingiliana na kila umahiri mahususi ndani ya umahiri mkuu wa kuwasiliana katika miktadha mbalimbali na umahiri mkuu wa kusoma kwa ufahamu katika kujenga uwezo wa kujieleza kwa namna mbalimbali.

**Jedwali la Maudhui ya Muhtasari**

| Umahiri Mkuu | Umahiri Mahususi | Shughuli za Kutendwa na Mwanafunzi | Vigezo vya Upimaji | Upimaji wa Viwango vya Utendaji | | | | Idadi ya Vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | *Utendaji wa awali wa Mwanafunzi* | *Utendaji wa wastani wa Mwanafunzi* | *Utendaji mzuri wa Mwanafunzi* | *Utendaji mzuri sana wa Mwanafunzi* | |
| 1. Kuwasiliana katika miktadha mbalimbali | 1.1 Kuanzisha na kuendeleza mazungumzo katika miktadha mbalimbali | a) Kutega na kutegua vitendawili na kuvihusianisha na vitu vilivyopo katika mazingira kwa usahihi | Vitendawili vimetegwa na kuteguliwa na kuhusianishwa na vitu vilivyopo katika mazingira | Anatega na kutegua vitendawili vichache sana na kuvihusianisha na vitu vilivyopo katika mazingira | Anatega na kutegua vitendawili vichache na kuvihusianisha na vitu vilivyopo katika mazingira | Anatega na kutegua vitendawili vingi na kuvihusianisha na vitu vilivyopo katika mazingira | Anatega na kutegua vitendawili vingi sana na kuvihusianisha na vitu vilivyopo katika mazingira kwa kutoa mifano | 38 |
| | | b) Kutamba ngonjera kwa kuzingatia kanuni za utambaji | Ngonjera inatambwa kwa kuzingatia kanuni za utambaji kwa usahihi | Anatamba ngonjera kwa kuzingatia kanuni chache sana za utambaji | Anatamba ngonjera kwa kuzingatia kanuni chache za utambaji | Anatamba ngonjera kwa kuzingatia kanuni nyingi za utambaji | Anatamba ngonjera kwa kuzingatia kanuni zote za utambaji na kuelezea umuhimu wake | |
| | | c) Kutumia nahau katika habari fupi na kuelezea maana zake | Nahau zinatumika katika habari fupi na kuelezewa maana zake kwa usahihi | Anatumia nahau chache sana katika habari fupi bila kuelezea maana zake | Anatumia nahau chache katika habari fupi na kuelezea maana zake | Anatumia nahau nyingi katika habari fupi na kuelezea maana zake | Anatumia nahau nyingi sana katika habari fupi na kufafanua maana zake kwa kutoa mifano | |

| Umahiri Mkuu | Umahiri Mahususi | Shughuli za Kutendwa na Mwanafunzi | Vigezo vya Upimaji | Upimaji wa Viwango vya Utendaji | | | | Idadi ya Vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Utendaji wa awali wa Mwanafunzi | Utendaji wa wastani wa Mwanafunzi | Utendaji mzuri wa Mwanafunzi | Utendaji mzuri sana wa Mwanafunzi | |
| | | d) Kutafsiri taswira inayoakisiwa na nahau | Taswira inayoakisiwa katika nahau inatafsiriwa kwa usahihi | Anatafsiri taswira inayoakisiwa katika nahau chache sana kwa kubahatisha ` | Anatafsiri taswira inayoakisiwa katika nahau chache | Anatafsiri taswira inayoakisiwa katika nahau nyingi | Anatafsiri taswira inayoakisiwa katika nahau nyingi kwa kufafanua na kutoa mifano | |
| | | e) Kutunga sentensi kwa kutumia kauli halisi | Sentensi zinatungwa kwa kutumia kauli halisi kwa usahihi | Anatunga sentensi chache sana kwa kutumia kauli halisi | Anatunga sentensi chache kwa kutumia kauli halisi | Anatunga sentensi nyingi kwa kutumia kauli halisi | Anatunga sentensi nyingi sana kwa kutumia kauli halisi | |
| | | f) Kutunga sentensi kwa kutumia kauli taarifa | Sentensi zinatungwa kwa kutumia kauli taarifa kwa usahihi | Anatunga sentensi chache sana kwa kutumia kauli taarifa | Anatunga sentensi chache kwa kutumia kauli taarifa | Anatunga sentensi nyingi kwa kutumia kauli taarifa | Anatunga sentensi nyingi sana kwa kutumia kauli taarifa | |
| | | g) Kueleza hatua za uandishi wa habari fupi/ insha | Hatua za uandishi wa habari fupi/insha zinaelezwa kwa usahihi | Anaeleza hatua chache sana za uandishi wa habari fupi/insha | Anaeleza hatua chache za uandishi wa habari fupi/insha | Anaeleza hatua nyngi za uandishi wa habari fupi/insha | Anaeleza hatua zote za uandishi wa habari fupi/ insha kwa kutoa mifano | |
| | | h) Kutumia nafsi tatu katika sentensi kwa kuzingatia hali ya umoja na wingi | Nafsi tatu zinatumiwa katika sentensi kwa kuzingatia umoja na wingi kwa usahihi | Anatumia nafsi chache sana katika sentensi kwa kuzingatia umoja na wingi | Anatumia nafsi chache katika sentensi kwa kuzingatia hali ya umoja na wingi | Anatumia nafsi tatu katika sentensi kwa kuzingatia hali ya umoja na wingi | Anatumia nafsi tatu katika sentensi kwa kuzingatia hali ya umoja na wingi na kuzifafanua | |

| *Umahiri Mkuu* | *Umahiri Mahususi* | *Shughuli za Kutendwa na Mwanafunzi* | *Vigezo vya Upimaji* | *Upimaji wa Viwango vya Utendaji* | | | | *Idadi ya Vipindi* |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | *Utendaji wa awali wa Mwanafunzi* | *Utendaji wa wastani wa Mwanafunzi* | *Utendaji mzuri wa Mwanafunzi* | *Utendaji mzuri sana wa Mwanafunzi* | |
| | 1.2 Kutumia msamiati katika kuzungumza kwa kuwasilisha hoja kulingana na muktadha mbalimbali | a) Kutunga sentensi kwa kutumia majina ya wanyama wanaofugwa na kuelezea faida zake | Sentensi zinatungwa kwa kutumia majina ya wanyama wanaofugwa na kuelezea faida zake kwa usahihi | Anatunga sentensi chache sana kwa kutumia majina ya wanyama wanaofugwa na kuelezea faida zake | Anatunga sentensi chache kwa kutumia majina ya wanyama wanaofugwa na kuelezea faida zake | Anatunga sentensi nyingi kwa kutumia majina ya wanyama wanaofugwa na kuelezea faida zake | Anatunga sentensi nyingi sana kwa kutumia majina ya wanyama wanaofugwa na kuelezea faida zake | 38 |
| | | b) Kusimulia hadithi fupi kwa kutumia majina ya wanyama wa porini | Hadithi inasimuliwa kwa kutumia majina ya wanyama wa porini na kuelezea sifa zao kwa ufasaha | Anasimulia hadithi kwa kutumia majina machache sana ya wanyama wa porini | Anasimulia hadithi kwa kutumia majina machache ya wanyama wa porini | Anasimulia hadithi kwa kutumia majina mengi ya wanyama wa porini | Anasimulia hadithi kwa kutumia majina mengi sana ya wanyama wa porini na kuelezea sifa zao kwa kutoa mifano | |
| | | c) Kufanya ziara nje ya darasa na kubaini majina ya maua tofauti yanayopatikana na kuelezea sifa zake | Majina ya maua tofauti yanabainishwa na kuelezewa sifa zake kwa usahihi | Anabainisha majina ya maua machache sana bila kuelezea sifa zake | Anabainisha majina ya maua machache na kuelezea sifa zake | Anabainisha majina mengi ya maua na kuelezea sifa zake | Anabainisha majina mengi sana ya maua na kuelezea sifa zake na yanakopatikana | |

| *Umahiri Mkuu* | *Umahiri Mahususi* | *Shughuli za Kutendwa na Mwanafunzi* | *Vigezo vya Upimaji* | *Upimaji wa Viwango vya Utendaji* | | | | *Idadi ya Vipindi* |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | *Utendaji wa awali wa Mwanafunzi* | *Utendaji wa wastani wa Mwanafunzi* | *Utendaji mzuri wa Mwanafunzi* | *Utendaji mzuri sana wa Mwanafunzi* | |
| | | d) Kuelezea shughuli za mwanafunzi anazotenda kila siku nyumbani kwa mpangilio | Shughuli za mwanafunzi anazotenda kila siku nyumbani zinaelezewa kwa mpangilio | Anaeleza shughuli chache sana za mwanafunzi anazotenda kila siku nyumbani | Anaeleza shughuli chache za mwanafunzi anazotenda kila siku nyumbani kwa mpangilio | Anaeleza shughuli nyingi anazotenda mwanafunzi nyumbani kwa mpangilio | Anaeleza shughuli nyingi sana anazotenda mwanafunzi kila siku nyumbani kwa mpangilio na kuandika habari fupi | |
| | | e) Kuelezea shughuli anazotenda mwanafunzi kila siku shuleni na kuandika habari fupi kwa mpangilio | Shughuli anazotenda mwanafunzi kila siku shuleni zinaelezwa na inaandikwa habari fupi kwa mpangilio | Anaeleza shughuli chache sana anazotenda mwanafunzi kila siku shuleni bila mpangilio | Anaeleza shughuli chache anazotenda mwanafunzi kila siku shuleni kwa mpangilio unaoeleweka | Anaeleza shughuli nyingi anazotenda mwanafunzi kila siku shuleni na kuandika habari fupi kwa mpangilio unaoeleweka | Anaeleza shughuli nyingi sana anazotenda mwanafunzi kila siku shuleni na kuandika habari fupi kwa mpangilio unaoeleweka | |
| | | f) Kuelezea muonekano wa hali ya hewa katika mazingira yake kikamilifu (ukungu, upepo, joto, baridi, mvua) | Mwonekano wa hali ya hewa katika mazingira yake unaelezewa kwa ufasaha | Anaelezea mwonekano wa hali ya hewa katika mazingira yake kwa kubahatisha | Anaelezea mwonekano wa hali ya hewa ya aina moja katika mazingira yake | Anaelezea mwonekano wa hali ya hewa ya ukungu, upepo, baridi, mvua na joto katika mazingira yake | Anaelezea na kufafanua mwonekano wa hali ya hewa ya aina zote na faida zake katika mazingira yake | |

| *Umahiri Mkuu* | *Umahiri Mahususi* | *Shughuli za Kutendwa na Mwanafunzi* | *Vigezo vya Upimaji* | *Upimaji wa Viwango vya Utendaji* | | | | *Idadi ya Vipindi* |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | *Utendaji wa awali wa Mwanafunzi* | *Utendaji wa wastani wa Mwanafunzi* | *Utendaji mzuri wa Mwanafunzi* | *Utendaji mzuri sana wa Mwanafunzi* | |
| | | g) Kutofautisha na kueleza vitu katika hali ya ukubwa na udogo wake | Vitu vinaelezewa na vinatofautishwa katika hali ya ukubwa na udogo wake kwa usahihi | Anatofautisha na kuelezea vitu vichache sana katika hali ya ukubwa na udogo kwa kubahatisha | Anatofautisha na kuelezea vitu vichache katika hali ya ukubwa na udogo | Anatofautisha na kuelezea vitu vingi katika hali ya ukubwa na udogo | Anatofautisha na kuelezea vitu vingi sana katika hali ya ukubwa na udogo | |
| | | h) Kuelezea idadi ya vitu vinavyohesabika katika umoja na wingi kwa kutumia sentensi kanushi | Vitu vinavyo hesabika vinaelezewa idadi yake katika umoja na wingi kwa kutumia sentensi kanushi kwa usahihi | Anaeleza idadi ya vitu vichache sana katika umoja na wingi katika sentensi kanushi | Anaelezea idadi ya vitu vichache katika umoja na wingi katika sentensi kanushi | Anaelezea idadi ya vitu vingi katika umoja na wingi katika sentensi kanushi | Anaelezea idadi ya vitu vingi sana katika umoja na wingi katika sentensi kanushi na kuonesha uelewa wa msamiati | |
| | 1.3 Kutumia maandishi katika kuwasiliana kulingana na miktadha mbalimbali | a) Kuandika vipengele vya muundo wa insha | Vipengele vya muundo wa insha vinaandikwa kwa mpangilio sahihi | Anaandika vipengele vichache sana vya muundo wa insha | Anaandika vipengele vichache vya muundo wa insha | Anaandika vipengele vingi vya muundo wa insha kwa mpangilio | Anaandika na kufafanua vipengele vyote vya muundo wa insha kwa mpangilio unaoeleweka | 19 |

| *Umahiri Mkuu* | *Umahiri Mahususi* | *Shughuli za Kutendwa na Mwanafunzi* | *Vigezo vya Upimaji* | *Upimaji wa Viwango vya Utendaji* | | | | *Idadi ya Vipindi* |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | *Utendaji wa awali wa Mwanafunzi* | *Utendaji wa wastani wa Mwanafunzi* | *Utendaji mzuri wa Mwanafunzi* | *Utendaji mzuri sana wa Mwanafunzi* | |
| | | b) Kuandika insha kuhusu umuhimu wa kuwa na familia ndogo | Insha kuhusu umuhimu wa kuwa na familia ndogo inaandikwa kwa usahihi. | Anaandika insha kwa kuzingatia vipengele vichache sana vya muundo wa insha | Anaandika insha kwa kuzingatia vipengele vichache vya muundo wa insha | Anaandika insha kwa kuzingatia vipengele vingi vya muundo wa insha | Anaandika insha kwa kuzingatia vipengele vyote vya muundo wa insha na matumizi sahihi ya alama za uandishi | |
